

HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO



UTARATIBU WA MAOMBI YA KUREKEBISHA MICHORO YA MIPANGOMIJI

Utaratibu wa kubadili matumizi unafanyika chini ya sheria Na. 8 ya Mipango Miji ya Mwaka 2007.

Hatua ya kwanza ni kuwasilisha barua ya maombi iliyosainiwa na mmiliki wa kiwanja ikieleza mambo yafuatayo:

1. Namba ya mchoro unaorekebishwa na mahali ulipo
2. Matumizi yaliyopo na makadirio ya ukubwa wa eneo
3. Matumizi ya viwanja baada ya marekebisho
4. Sababu za kuomba kurekebisha mchoro

VIAMBATANISHO

Maombi ya kurekebisha mchoro wa mipangomiji yanawasilishwa yakiwa na viambatanisho vifuatavyo;

1. Ramani ya upimaji kwa wale waliopima
2. Nakala ya Mchoro wa mipangomiji unaokusudiwa kurekebisha
3. Nakala za Risiti za kodi ya majengo kama kuna jengo

HATUA

1. Ukaguzi wa eneo

2. Kuandaa taarifa ya kitaalamu pamoja na mchoro
3. Kuwasilishwa kwenye kikao cha kamati ya mipangomiji na mazingira kwa ajili ya kujadiliwa
4. Kuwasilisha Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa
5. Kuwasilisha Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kupata Idhini.